**MKURABITA NYEZO YA SERIKALI INAYOIBUKIA KUWAWEZESHA WANYONGE WALIO WENGI NCHINI: KUJENGA UWEZO WA HALMASHAURI ZA WILAYA**

**Utangulizi:**
Kufuatia kukamilika kwa Awamu ya Uandaaji wa Maboresho Julai 2008, MKURABITA iliingia katika awamu yake ya Tatu ambayo ni Utekelezaji wa Maboresho. Menejimenti ya MKURABITA ilianza kwa kutekeleza baadhi ya mapendekezo hayo yanayo husiana na urasimishaji wa rasilimali vijijini na hata mijini kwa utaratibu iliyoita "**FRONT RUNNERS**" kwa mbinu ya Ujengeaji uwezo Halmashauri za wilaya. Katika utaratibu huu MKURABITA ilianza na wilaya kumi ambazo ni Makete, Njombe, Wete, Musoma, Serengeti, Manyoni, Mpwapwa, Mvomero, Rufiji na Nachingwea.

Kabla ya kuingia uwandani katika wilaya hizi kumi, MKURABITA ilianza na mfululizo wa majadiliano kupitia vikosi kazi vinavyojumuisha wawakilishi toka katika wizara, idara na taasisi pamoja na wadau mbalimbali kujenga muafaka na makubaliano ya msingi juu ya mapendekezo yaliyoandaliwa. Hatua hii ina lenga katika la kuwashirikisha wadau husika ili wayakubali na kuona ni sehemu ya yale wanayopaswa kuyatekeleza katika shughuli zao za kila siku hasa idara zenye dhamana ya masuala haya. Miongoni mwao ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na baadhi ya Wakala wa Serikali.

Vikosi kazi vilivyoundwa ili kusaidia katika kuongeza msukumo wa utekelezaji wa mapendekezo haya na vinaendelea vizuri katika kukamilisha shughuli walizokabidhiwa. Kkama ilivyo kwa upande wa urasimishaji wa rasilimali, mashauriano na maandalizi juu ya Urasimishaji wa Biashara yanaendelea.

Pamoja na mapendekezo na makubaliano yaliyoafikiwa katika mfululizo wa mashauriano haya hadi hivi sasa shughuli kadhaa zimebainishwa kwa utekelezaji wa maboresho. Hii ni pamoja na kuundwa kwa timu ya wakurufunzi wa wakufunzi (Trainer of trainers -TOT) inayosimamiwa na MKURABITA. Timu hii inajumuisha wataalam toka Wizara ya Ardhi, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Vyuo Vikuu Ardhi na Dar es Salaam-DUCE na baadhi kutoka halmashauri za wilaya na manispaa pamoja na sekta binafsi. Hii ndio timu inayoendesha zoezi la kuzijengea uwezo halmashauri za wilaya katika wilaya kumi za awali.Baada ya kuundwa timu hii ilipata mafunzo ambayo yanalenga katika maeneo makuu matatu ikiwemo MKURABITA na maboresho yaliyoandaliwa pamoja na sheria za ardhi na matumizi bora ya ardhi.

**Utekelezaji wa zoezi la kuzijengea uwezo halmashauri za wilaya:**
***Sababu za kujenga uwezo katika halmashauri za wilaya:***
Ni jambo la msingi kujenga uwezo wa halmashauri katika kutekeleza mchakato wa urasimishaji hasa urasimishaji wa rasilimali kwani halikwepeki kwa sababu Sheria

ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007 imezipa halmashauri za wilaya jukumu la kusimamia urasimishaji wa ardhi ya vijiji na uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini. Hata hivyo uzoefu umeonyesha kuwa karibu wilaya zote hazijaweza kutumia asilimali zao kuendesha shughuli za urasimishaji ardhi wala kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Aidha imeonekana kwamba sheria zote mbili zimeweka masharti ambayo ni magumu kwa Halmashauri nyingi kuyatimiza. Moja ya masharti hayo ni ile inayozitaka halmashauri za wilaya lazima ziwe na masjala ya ardhi ya wilaya ili iweze kurasimisha ardhi. Na kwa matumizi bora ya ardhi ni lazima timu ya wilaya iundwe ambayo itashirikiana na vijiji kuandaa mipango.

Katika kufanya kazi na halmashauri uzoefu wa MKURABITA umeonyesha kwamba halmashauri za wilaya nyigi hazitengi bajeti kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi. Tangu Sheria Na. 5 ianze kutumika mwaka 2001 ni Halmashauri ya wilaya ya Mbozi, Handeni, Monduli, Babati, Kiteto, na iringa ndio zilizoanza urasimishaji kwa msaada wa wizara ya Ardhi, GTZ na NGOs za Arusha.

Vile vile halmashauri za wilaya nyingi hazina vifaa kama vile GPS Satellite Recivers, Computers, Printers, kamera, lamitating machines, Vitabu vya Usajili Ardhi na wataalam wakutosha waliofundishwa mchakato wa Urasimishaji ardhi na uandaaji wa Mipango ya matumizi bora ya Ardhi.kuendesha zoezi la urasimishaji ardhi. Kutokana na hali halisi kwamba halmashauri hazina bajeti kwa urasimishaji ardhi hela kwa ajili ya mafuta na posho za watendaji kwenda vijijini hakuna na zoezi hili pia halifanyiki.

Hii ikiwa ndiyo hali halisi, ikumbukwe kwamba Tanzania ina zaidi ya halmashauri za wilaya zapatazo ----. Hivyo kuzifikia zote jitihata na mkakati maalum unahaitajika. Ni kutokana na kuliona hili MKURABITA iliona ni vyema kuufanya mchakato wa urasimishaji uwe endelevu na hapana budi kwa serikali na wadau wake kuzijengea halmashauri za wilaya uwezo wa kutekeleza mpango huu wa urasimishaji rasilimali hasa kwa vijijini.

**Kujenga uwezo wa Halmashauri za Wilaya**
Katika utekelezaji wa zoezi hili timu ya MKURABITA huanza kwa kukutana na uongozi wa Mkoa hasa Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa ili wafahamu uwepo wa shughuli hizo katika katika mkoa wao na kushiriki kikamilifu na kuingiza katika mipango yao ya mkoa hapo baadaye. Baadaye Timu huenda wilayani ambapo hukutana na viongozi kama vile Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya, Mkuregenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa halmashauri na vongozi wengine. Katika Kikao hiki maelezo yote ya kina yanayohusu Mpango huu huelezwa na hatimaye ratiba huandaliwa kiwilaya.

Timu hii ikiwa huko wilayani huendesha zoezi hili kama ifuatavyo**:-**
***a. Mikutano ya Uhamasishaji:***

Timu ya MKURABITA huendesha mikutano ikiwemo kikao kinachohusisha Madiwani wa Kata zinazohusika na vijiji vilivyo katika Mpango na wakuu wote wa idara wilayani. Katika kikao hiki mambo yafuatayo hufanyika:

- Kutoa ufahamu kwa kuelezea kwa muhtasari juu ya **MKURABITA** kwa ujumla. Hivyo washiriki kuelewakwa kina juu ya **Dhana ya MKURABITA** ambayo imelenga katika uwezeshaji wa wananchi kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali na vipaji, kushiriki katika shughuli za uchumi wa soko zinazoendelea nchini. Pia wajumbe hupata ufafanuzi juu ya Uhusiano wa MKURABITA na MKUKUTA pamoja na Mipango mingine.

  Aidha washiriki wa kikao hiki hupata maelezo juu ya suala zima la uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi hatua ambayo ni muhimu katika mchakato wa urasimishaji ardhi vijijini ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali ardhi. Hivyo ufafanuzi hutolewa kwa washiriki ili kutoa msisitizo juu ya faida za kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi na si bora matumizi kwa sababu:
  - Mpango wa matumizi bora ya ardhi ni utaratibu wa tathmini ya uwezo wa ardhi na maji, unaojumuisha chaguzi mbadala za matumizi ya ardhi na hali ya uchumi na jamii ili kuchagua na kutumia aina au njia bora za matumizi ya ardhi.
  - Huwezesha kupunguza na kudhibiti kuongezeka kwa idadi ya migogoro isiyo ya lazima miongoni mwa watumiaji wa ardhi.
  - Huondoa hofu na shaka la kutokuwa na uhakika wa miliki na matumizi ya ardhi kwa kuandaa na kutoa Hati Miliki za Ardhi za Kimila (CCROs) ambazo huwapa wamiliki uhakika na usalama wa miliki zao.
  - Huondoa dhana iliyojengeka kwa wananchi walio wengi juu ya maendeleo duni ya soko la ardhi lisilo rasmi.
  - Hudhibiti uharibifu wa ardhi/udongo na vyanzo vya maji.
  - Hudhibiti ufyekaji holela na uchomaji misitu na matumizi mengine mabaya ya rasilimali hii
  - Hudhibiti ongezeko la kuhamahama kwa watu na mifugo na hatimaye kuzuia kuongezeka kwa ukame na tishio la jangwa.

Pamoja na maelezo juu ya MKURABITA na Umuhimu wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, wajumbe hupata nafasi ya kuelimika juu ya sheria zinazohusiana na masuala ya ardhi zikiwemo ***Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999***, ***Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999***, ***Sheria ya Matumizi ya Ardhi namba 6 ya Mwaka 2007***, Sheria ya Madini, Mazingira, Sheria ya Mahakama za Ardhi na Utatuzi wa Migogoro na nyingine zinazohusika na masuala ya ardhi kwa ujumla**.**

Ni katika Mkutano huu ambapo Halmashauri ya Wilaya huteua Timu ya Wataalamu kutoka ngazi ya Wilaya na Kata ilikuwezesha kuanza na kufanyika kwa Mchakato wa urasimishaji vijijini. Timu hii hujumuisha wataalmu wa fani na idara mbalimbali zikiwa ni pamoja na idara ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Mali asili, Maendeleo ya Jamii, Ujenzi/Miundo mbinu, Afya, Maji, Elimu, Sheria na Mipango. Katika ngazi ya Wilaya hupendekezwana kuthibitisha majina ya vijiji

vitakavyohusika na mchakato pamoja na majina ya wataalamu kumi (10) na katika kila kata husika huchaguliwa wataalamu wapatao watano (5).

b. ***Mafunzo na Kujengea Uwezo Timu ya Wilaya na Kata (PLUM & WLUM Teams):***
Hii ni hatua ya pili katika zoezi linaloendeshwa na Timu ya MKURABITA ikiwa wilayani baada ya kikao cha wakuu wa idara kupendekeza na kuyathibitisha majina ya wanaonda timu ya PLUM na WLUM ambapo hutoa mafunzo ambayo huchukua takriban siku nne hadi tano ikijumuisha mafunzo juu ya utumiaji wa teknolojia rahisi na ya kisasa Katia upimaji yaani 'matumizi ya ***Hand held GPS'***.

Wataalamu walioteuliwa kutoka ngazi ya wilaya na kata hupata mafunzo juu ya **MKURABITA**, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Sheria za Ardhi, Upimaji, Uhakiki, Utatuzi wa migogoro ya miliki, Uandaaji na Utoaji wa Hati Miliki za Ardhi za Kimila (CCROs), Uendeshaji wa Masjala za Ardhi za Wilaya na Vijij, Utumiaji wa GPS na mfumo wa habari za kijiografia (GIS) katika kuandaa ramani za aina mbalimbali ikiwemo upimaji wa mashamba na uandaaji wa vyeti vya ardhi vya vijiji na Hati Miliki za Kimila.



c. ***Kutembelea na Kubaini Vijiji Vinavyohusika na Utekelezaji wa Urasimishaji***
Timu za wilaya na kata zikongozwa na timu ya MKURABITA hufanya ziara ya kutembelea na kubaini kwa undani vijiji vilivyopendekezwa na halmashauri ya wilaya kuhusika na utekelezaji wa Mpango, lengo likiwa ni kupata uzoefu na ufahamu zaidi juu ya vijiji husika, kuangalia kijiji kinachofaa kutumika kama kijiji darasa (practicum village), pamoja na kujua miundo mbinu iliyopo na mf. Ofisi za serikali za vijiji na masjala ya ardhi ya kijiji. Pia timu hizo hufanya mikutano ya uhamasishaji katika ngazi ya kitongoji na vijiji ili kufikisha wananchi walio wengi.



*Ofisi ya Kijiji cha Namatunu, Nachingwea. Vijiji vingi havina ofisi na zilizopo ziko katika hali mbaya*

d. ***Kuzindua Mchakato wa Urasimishaji kwa njia ya mafunzo kwa vitendo ngazi ya Kijiji***
Madhumuni ya hatua hii ni kuzijegea uwezo Timu za Wilaya, Kata na Vijiji ili ziweze kufikia na kutimiza lengo katika mchakato wa urasimishaji kwa kuzingatia vipengele vikuu vifuatavyo:-

- Kuandaa na ama kurejea Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji
- Kuandaa mifumo/miundo ya kitaasisi ya Kijiji kama vile:
  - Baraza la Ardhi la Kijiji

- Kamati ya Usimamizi wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji.
- Kamati ya Uhakiki wa Maslahi ya Ardhi ya Kijiji
- Kuteua Mshauri wa Kamati ya Uhakiki
- Kumwezesha Afisa Mtendaji wa Kijiji kuwa Msajili wa Hati Miliki za Kimila (CCROs) za ardhi kijijini.
- Kuanzisha Masjala ya Ardhi ya Kijiji (Village Land Registry-VLR).

- Kuwezesha utaratibu wa uchukuaji na ujazaji wa fomu za maombi ya ya kupimiwa ardhi na kupata Hati Miliki ya Kimila kwa wamiliki pamoja na suala zima la uanzishaji wa masjala ya ardhi ya kijiji (**Village Land Registry –VLR**).
- Kuwezesha upitishaji wa maombi, kupima, kuhakiki mashamba, kutatua migogoro ya mipaka na miliki, upigaji wa picha, uandaaji wa ramani na hati, usajili na utoaji wa Hati Miliki za Kimila.
- Kutoa mafunzo kwa wanakijiji wanaochaguliwa juu ya utumiaji wa GPS kwa ajili ya upimaji katika kijiji husika (assistant surveyors)
- Kuhamasisha jamii juu ya ushiriki wao na umuhimu wa ujenzi wa masjala za ardhi za vijiji kwa vile ambavyo ofisi zilizopo zina hali mbaya na haziwezi kutumika kama masjala za ardhi za vijiji



*Moja ya mikutano ya uhamasishaji ngazi ya kitongoji-Kitongoji cha Chang'ombe, Manyoni*

Hatua hizo ndizo zilizofanyika katika wilaya kumi na mbili zilizowezeshwa na MKURABITA kupitia utaratibu wa ***Kijiji Darasa kama vile Mbondo (Nachingwea) Sajaranda (Manyoni), Kyankoma na Nyakiswa (Musoma),***

***e. Uanzishaji na Ukarabati wa Masjala:***

MKURABITA kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya na jamii katika vijiji vinavyobainishwa katika utekelezaji wa Mpango huu inawezesha ujenzi, ukarabati na uanzizhwaji wa masjala za ardhi katika wilaya na vijiji. Aidha MKURABITA katika ngazi ya wilaya masjala huwezesha ujenzi pale ambapo wilaya haina ofisi ya masjala pamoja na ukarabati na kuanzishwa kwa maabara ambazo hupatiwa vifaa kama vile Computer yenye programu za uchoraji wa ramani na GIS kwa ujumla, printer 1, Laminator 1, Camera 1, Hand held GPS 10 na makaratasi ya Crested.

Katika ngazi ya kijiji MKURABITA inawezesha upatikanaji wa shajala zote muhimu kama vile: majalada, reja, punch, steppler, vidau vya kuwekea wino wa mihuri pamoja na fomu za kutosha za maombi ya wa miliki kupimiwa mashamba, hizo waombaji wanapaswa kuchangia gharama kidogo za utayarishaji wa hati miliki za kimila kiasi cha shilingi elfu mbili na mia tano (2,500/=).

Katika ujenzi mzima wa masjala hizo za ardhi za vijiji na hata wilaya, MKURABITA inachangia gharama za fundi, vifaa vya ujenzi katika masjala

zinazojengwa na zinazokarabatiwa (sementi, bati, nondo na ceiling boards na makabineti). Hivyo Halmashauri za wilaya na za vijiji husika na ujenzi wa masjala za ardhi za vijiji zinahimizwa kufungua akaunti maalum kwa ajili ya ujenzi ili kuimarisha utamaduni wa uwazi na uwajibikaji pamoja na utawala bora.

Katika hatua hii wananchi wao huchangia nguvu kazi katika kukusanya mchanga, mawe, kokoto, maji na kufyatua tofali na vibarua wakati wa ujenzi. Jukumu la Halmashauri ya Wilaya huwa ni kusimamia na ushauri, kutoa wataalam wake pamoja na usafiri kwa vifaa vya ujenzi kwenda eneo la ujenzi pia kuhakikisha upatikanaji wa vifaa eneo la ujenzi kwa wakati.

**Wilaya zilizofikiwa na kujengewa uwezo na M KURABITA:**
Katika dhana hii ya ujengeaji uwezo halmashauri za wilaya kwa mwaka huu wa fedha MKURABITA imekwisha wezesha zoezi hili katika wilaya kumi na mbili na vijiji sabini na mbili ambavyo ni:


- **Handeni**- (***vijiji 7***) Sindeni, Mzeri, Kweisasu, Bongi, Nkale, Mbuyuni na Kwamkono. Wakati wa Uandaaji wa Maboresho (Wilaya hii ilihusishwa kwa ajili ya Uhakiki wa Maeneo kwa Uamuzi Maalum wakati wa uandaaji wa mapendekezo ya maboresho)-Lengo lilikuwa kutathmini kazi ya urasimishaji kwa kutumia sheria ya ardhi ya vijiji jinsi ilivyo
- **Bagamoyo**- (***vijiji 6***) Fukayosi, Kiwangwa, Msinune, Masugulu, Kihangaiko na Msoga. Wakati wa Uandaaji wa Maboresho Wilaya ilihusishwa katika Uhakiki wa Mpangilio. Lengo lilikuwa kutahmini uhakiki wa mpangilio kwa kutumia sheria jinsi ilivyo kulingana na mapendekezo ya maboresho
- **Musoma Vijijini** (vijiji 8) Kyankoma, Suguti, Wanyere, Chirorwe, Butiama, Buturu, Nyakiswa na Mwimbagi. **Serengeti** (vijiji 5) Park Nyigoti II, Robanda, Nattambiso, Makundusi na Nyichoka. **Njombe Mjini,** Idunda, Yakobi, Iboya, Kifanya, Kilenzi, Iwungilo, Kisilo, Igoma (vijiji 8) na **Makete** (vijiji 5) Mwakauta, Iniho, Kidope, Mang'oto na Malembuli (Baada ya Maboresho)
- **Wete** (Pemba) shehia ya Kiungoni (vijiji 4) Kivugo, Chonyi, Kiungoni, na Kimango, **Rufiji** (vijiji 10) Nyamwage, Mbwara, Mchukwi A, Kivinja B, Nyamisati, Jaribu Mpakani, Kilimani Mashariki, Kilulatambwe, Kikale na Mng'aru. **Nachingwea** (vijiji 6), **Mpwapwa** (vijiji 7), Idaho, Pwaga, Munguwi, Mwenzele, Tambi, Inzomvu na Mlembule **Manyoni** (vijiji 3), Sanjaranda, Kitopeni na Gurungu na **Mvomero** (vijiji 6) Lubungo, Melela, Kimambira, Maharaka, Mangae na Manza (Baada ya Maboresho)

**Tija na Ufanisi katika utekelezaji wa Urasimishaji vijijini**

- Baada ya halmashauri kujengewa uwezo jukumu kuu la ya PLUM ngazi ya wilaya ni kutoa muongozo wa kiufundi na kufuatilia utendaji na pamoja na kutoa mafunzo kwa timu za kata. Timu ya GIS ya wilaya inafanya kazi uwandani ili kuongeza kasi ya uingizaji wa mashamba na kuandaa hati miliki za kimila kwa muda muafaka

Aidha timu za kata zinakuwa na jukumu la kusaidiana na halmashauri za vijiji katika kuandaa mipango wa matumizi bora ya ardhi, Kuhakiki wamiliki na

kupima mashamba ya wamiliki. Hawa husaidiana na wapima wasaidizi ambao hupima maeneo ya mpango pamoja na kupima mashamba ya wananchi wanao yamiliki.




**MKURABITA imejifunza nini katika zoezi hili:**

- Kuna haja ya kuwa na Nyaraka zilizosawa (standardized) kwa ajili ya kutumiwa na timu ya kitaifa kwenye wilaya zote
- Kuna haja ya kupunguza gharama za urasimishaji ili tufikie viwango vya kimataifa (kila hati isizidi gharama ya dola za Kimarekani 10). Sasa hivi wastani ni dola za Kimarekani 25

**Changamoto na Fursa zilizopo:**

- Kujenga uwezo wa Halmashauri kunahitaji fedha nyingi na muda mrefu pia
- Halmashauri hazitengi bajeti kwa ajili ya urasimishaji hivyo kuna haja sasa ya kuhamasisha Halmashauri zote zianze kutenga bajeti kwa shughuli hii
- Suala la ujenzi wa Masjala za ardhi vijijini linahitaji kukubalika na TAMISEMI na suala hili liingizwe katika mipango ya kila Halmashauri ya wilaya.

**Mipango ya baadaye:**

- Kuibua mabadiliko/maboresho mapya kutokana na uzoefu wa uwandani
- Kutafuta mbinu za kuongeza mitaji kwa wanaorasimisha rasilimali zao
- Kufanya jitihada za makusudi zifanyike katika kukuza soko la rasilimali ardhi (property market development)